**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA MWANZA**
**MTIHANI WA UTAMILIFU KIDATO CHA PILI**

**021**

# KISWAHILI

**Muda: 2:30** **Mwaka 2025**

## MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi (10)**
2. Jibu maswali yote
3. Sehemu **A** na **C** zina alama **kumi na tano (15)** kila moja, na sehemu **B** ina alama **sabini (70)**
4. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali
5. Majibu yote yaandikwe kwenye nafasi ulizopewa
6. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa bluu au mweusi
7. Vifaa vyote vya mawasiliano visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha upimaji.

| KWA MATUMIZI YA UPIMAJI TU | | |
|---|---|---|
| **NAMBA YA SWALI** | **ALAMA** | **SAHIHI YA MPIMAJI** |
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |
| **JUMLA** | | |
| | **SAHIHI YA MHAKIKI** | |

Mtihani huu una kurasa **8** zilizochapwa

## SEHEMU A: (ALAMA 15)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Katika vipengele (i) hadi (x), chagua jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu hilo katika kisanduku ulichopewa.

(i) Neno "walimpigania" lina mofu ngapi?

A. Tano B. Saba

C. Sita D. Nne ( )

(ii) Ufahamu wa kusikiliza hutokana na mambo mawili ni yapi hayo?

A. Kusoma na kuandika

B. Kusomewa hadithi na kuona tukio ( )

C. Kusimuliwa hadithi na kusoma hadithi

D. Kusomewa habari na kusimuliwa hadithi

(iii) "Mazingara ya shule yanavutia sana." Kosa la kisarufi katika tungo hii limetokana na nini?

A. Kuongeza viambishi B. Kutozingatia matamshi ( )

C. Kuchanganya msamiati D. Kuacha maneno

(iv) Kipi kati ya vifuatavyo <u>si</u> kipera cha maigizo?

A. Mizungu B. Utani ( )

C. Majigambo D. Miviga

(v) Mayombya amekwenda <u>**kwa**</u> Juma. Neno lililopigiwa mstari ni aina gani ya neno?

A. Kihusishi B. Kiunganishi ( )

C. Kivumishi D. Kielezi

(vi) Alama za uandishi, matamshi sahihi ya maneno na kasi stahiki katika usomaji husaidia nini kwa msomaji?

A. Kujenga hoja B. Kuchochea ari ya kusoma ( )

C. Kupenda kusoma D. Kuelewa kile kinachozungumziwa

(vii) Upi ni mfano wa tafsida kati ya tungo zifuatazo?

A. Salma amejifungua. B. Ndege wanaimba kwa furaha. ( )

C. Sikitu ni mzuri kama malaika. D. Musa ni mkaa.

(viii) Ni kipengele kipi cha fani huonesha msuko wa visa na matukio katika kazi ya fasihi?

A. Mtindo B. Muundo ( )

C. Lugha D. Wahusika

(ix) Ni kipengele kipi <u>si</u> sehemu ya muundo wa barua isiyo rasmi?

A. Jina la mwandishi B. Anwani ya mwandishi ( )

C. Kimalizio cha barua D. Saini ya mwandishi

(x) Yafuatayo ni mambo ya kuzingatia katika uandishi wa aina yoyote ile, **isipokuwa**:

A. Kujua lugha nyingi

B. Kuelewa vyema jambo unaloliandikia ( )

C. Kufuata mtiririko mzuri wa mawazo

D. Kutumia lugha fasaha

2. Oanisha maelezo yaliyo katika **Orodha A** na dhana husika katika **Orodha B**, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika jedwali ulilopewa.

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| (i) Msimuliaji au mwasilishaji wa kazi ya fasihi<br>(ii) Wasikilizaji au wasomaji wa kazi ya fasihi<br>(iii) Mchambuzi wa kazi ya fasihi<br>(iv) Mtunzi wa mashairi<br>(v) Mhusika shujaa katika kazi ya fasihi. | A. Malenga<br>B. Fanani<br>C. Mhakiki<br>D. Mfoili<br>E. Jagina<br>F. Hadhira<br>G. Tahakiki |

Majibu

| **Orodha A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Orodha B** | | | | | |

**SEHEMU B: (ALAMA 70)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Soma habari ifuatayo kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata:

Bota ni mtoto wa kiume katika familia ya Mzee Bure aliyezaliwa na kulelewa katika mazingira ya kijijini. Baada ya **kuhitimu** elimu ya msingi, hakubahatika kuchaguliwa kuendelea na elimu ya sekondari kwa kuwa hakufanya vizuri katika mitihani yake. Suse, mama yake Bota, alimshauri mumewe wampeleke kijana wao katika shule ya binafsi ili aweze kupata elimu ya sekondari. Bure alionesha **kusita** kwa kuwa hakuwa na uwezo mzuri kifedha. Hata hivyo, kutokana na **ushawishi** wa mkewe, alikubali ushauri huo na akauza ng'ombe mmoja aliyekuwa naye kisha akampeleka mtoto wake shuleni.

Kutokana na hali ya uchumi kuwa ngumu, wakati mwingine Bota alichelewa kwenda shuleni kwa sababu ya kukosa ada. Mama yake aliumizwa sana na hali hiyo; hivyo akaamua kuanzisha biashara ya kuuza samaki. Aliuza samaki hao kwa kubadilishana na mazao na kisha akauza mazao hayo na kujipatia fedha. Kila faida aliyoipata aliielekeza katika kumsomesha Bota. Baba yake pia alijitahidi kufanya kazi zake kwa bidii ili kwa pamoja, wapate fedha za kumsomesha mtoto wao. Maisha yalizidi kuwa magumu kwani kuna wakati walikula mboga bila chumvi na kuoga bila sabuni ili tu Bota apate ada na mahitaji ya shule.

Baada ya kuhitimu kidato cha nne, Bota alichaguliwa kujiunga na chuo cha uvuvi ambako alihitimu mafunzo yake. Alipomaliza, hakusubiri kuajiriwa na serikali bali aliamua kujiunga na kikundi cha vijana wajasiriamali. Alichukua mkopo kwenye kikundi chake akanunua zana za uvuvi na kuamua kujiajiri kwenye sekta ya uvuvi.

Mungu si athumani, biashara ya uvuvi ilimletea **tija** kwani Bota alipata mtaji mkubwa kiasi cha kuweza kusafirisha samaki ndani na nje ya nchi. Maisha ya ke na ya familia yake yakabadilika na kuwa mazuri. Aliweza kupata fedha za kuwajengea wazazi wake nyumba nzuri na kununua gari. Wazazi wake walikumbuka maisha ya awali na kusema, "Ama kweli, mchumia juani hulia kivulini."

**Maswali:**

(a) Pendekeza kicha cha habari hii kwa maneno yasiyopungua matano.

.................................................................................................

(b) Habari hii inahusu nini?

.................................................................................................

.................................................................................................

.................................................................................................

(c) Kama ungekuwa mzazi wa Bota, ungefanya nini baada ya Bota kutochaguliwa kujiunga na masomo ya sekondari?

.................................................................................................

.................................................................................................

.................................................................................................

(d) Fafanua maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa na mwandishi wa habari hii.

(i) Kuhitimu ..........................................................................

.................................................................................................

.................................................................................................

(ii) Kusita ..........................................................................

.................................................................................................

.................................................................................................

(iii) Ushawishi: ..........................................................................

.................................................................................................

.................................................................................................

(iv) Tija: ..........................................................................

.................................................................................................

.................................................................................................

(e) Mtunzi anamaanisha nini anaposema "Mchumia juani hulia kivulini"?

.................................................................................................

.................................................................................................

.................................................................................................

4. (a) Eleza maana ya "uundaji wa maneno"

.................................................................................................

.................................................................................................

.................................................................................................

(b) Kwa kutoa mifano, fafanua dhana zifuatazo:

(i) Mofu

.................................................................................................

.................................................................................................

(ii) Mofimu

.................................................................................................

.................................................................................................

(iii) Alomofu

................................................................................................

................................................................................................

................................................................................................

(iv) Fonimu

................................................................................................

................................................................................................

................................................................................................

(v) Akronimu

................................................................................................

................................................................................................

................................................................................................

5. (a) Nini maana ya utata?

................................................................................................

................................................................................................

................................................................................................

(b) Tungo zifuatazo ni tata. Kwa kila tungo uliyopewa, onesha chanzo cha utata.

(i) Nipe sahani ya kulia.

................................................................................................

................................................................................................

................................................................................................

(ii) Kesho mtakuja na nyanya

................................................................................................

................................................................................................

................................................................................................

(iii) Mtoto alilalia uji.

................................................................................................

................................................................................................

................................................................................................

(iv) Musa alipigiwa mpira.

................................................................................................

................................................................................................

................................................................................................

(v) Joni anawachezea wanangu.

................................................................................................

................................................................................................

................................................................................................

6. (a) Toa maana ya “kiimbo”

................................................................................................

................................................................................................

................................................................................................

(b) Kiimbo kina dhima mbalimbali katika mawasiliano. Thibitisha kauli hii kwa hoja **tano (5)**.

(i) ..................................................................................................
..................................................................................................

(ii) ..................................................................................................
..................................................................................................

(iii) ..................................................................................................
..................................................................................................

(iv) ..................................................................................................
..................................................................................................

(v) ..................................................................................................
..................................................................................................

7. (a) Fafanua dhana ya "uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi"

..................................................................................................
..................................................................................................
..................................................................................................

(b) Neema ni mwimbaji wa nyimbo za Kiswahili ambaye huhifadhi nyimbo zake katika mtandao wa kijamii wa "YouTube." Fafanua hasara **tano (5)** ambazo zinaweza kujitokeza kutokana na kuhifadhi nyimbo zake kwa njia hii.

(i) ..................................................................................................
..................................................................................................

(ii) ..................................................................................................
..................................................................................................

(iii) ..................................................................................................
..................................................................................................

(iv) ..................................................................................................
..................................................................................................

(v) ..................................................................................................
..................................................................................................

8. (a) Eleza kiufupi umuhimu wa wahusika katika fasihi simulizi.

..................................................................................................
..................................................................................................
..................................................................................................
..................................................................................................

(b) "Fasihi simulizi ina wahusika wa aina **tano**." Thibitisha.

(i) ..................................................................................................

(ii) ..................................................................................................

(iii) ..................................................................................................

(iv) ..................................................................................................

(v) ..................................................................................................

9. Chukulia wewe unaitwa Faraja Malifedha unayesoma katika shule ya Sekondari Muungano iliyoko mjini Kahama. Una kaka yako aitwaye Baraka Malifedha anayeishi mkoani Arusha. Mwandikie ujumbe wa simu ya maandishi wenye maneno **kumi (10)** kumtaarifu kuwa unaumwa, hivyo akutumie pesa ya matibabu.

**SEHEMU C : (ALAMA 15)**

Jibu swali la **kumi (10)**

10. Jifanye wewe ni Amani Furaha unayesoma katika shule ya Sekondari Upendo iliyoko wilayani Sengerema. Unatarajia kusherekea kumbukizi ya siku ya kuzaliwa kwako tarehe 16 Oktoba, 2025. Andika barua ya mwaliko wa tukio hilo utakayoituma kwa rafiki yako aitwaye Riziki Mtwaro.